ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 40*** ***2nd October, 2020***

## *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No 40. Vol.101 dated 2nd October, 2020*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA 839 la tarehe 2/10/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

------------------
*(zmetungwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16 (1))*
----------------------------

SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA ZA MWAKA 2020

Jina

**1**. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za Mwaka 2020.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia

Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Mkurugenzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa ada na ushuru

**4.-** (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

(5) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (4), Halmashauri inaweza kukubaliana na walipa ushuru wakubwa kuweka utaratibu maalum wa kulipa ushuru.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

**5.** Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

**6.-** (1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(4) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

**7.-** (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali

au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata.mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

**8.-** (1) Halmashauri inaweza kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**9.** Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

**10.-** (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi; au

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri au shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) atahukumiwa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne.

Kufililisha kosa

**11.** Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

# JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 4(1))*

## SEHEMU A

### USHURU WA KUEGESHA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA.

| | AINA YA GARI | USHURU KWA SIKU |
|---|---|---|
| **1.** | Gari / basi kubwa | Tshs 1500/= |
| **2.** | Magari madogo (hiace) | Tshs 1000/= |
| **3.** | Taxi | Tshs 500/= |
| **4.** | Pikipiki | Tshs 200/= |
| **5.** | Magari binafsi yasiyo ya biashara | Tshs 500/= |
| **6.** | Gari dogo la mizigo (lori au pick up)chini ya tani 7 | Tshs 2000/= |
| **7.** | Gari kubwa la mizigo zaidi ya tani 7 | Tshs 3000/= |

## SEHEMU B
### ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

| | AINA YA MIFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| **1.** | Ng’ombe | Tshs 2000/= |
| **2.** | Mbuzi | Tshs 1000/= |
| **3.** | Kondoo | Tshs 1000/= |
| **4.** | Nguruwe | Tshs 2000/= |

## SEHEMU C

## USHURU KATIKA MASOKO, NA MAGULIO/MINADA.

| | AINA YA BIASHARA | USHURU KWA SIKU |
|---|---|---|
| **1.** | Biashara ya nguo za mitumba | Tshs 1,000/= |
| **2.** | Biashara za nguo za madukani | Tshs 1,000/= |
| **3.** | Biashara ya viatu vya mitumba | Tshs 1,000/= |
| **4.** | Biashara ya mama lishe | Tshs 1,000/= |
| **5.** | Biashara ya vileo | Tshs 1,000/= |
| **6.** | Biashara ya kuuza nyama | Tshs 1,000/= |
| **7.** | Michezo mbalimbali katika soko | Tshs 1,000/= |
| **8.** | Biashara za bidhaa za urembo | Tshs 1,000/= |
| **9.** | Biashara ya vyombo vya ndani | Tshs 1,000/= |
| **10.** | Biashara ya samaki mbalimbali | Tshs 1,000/= |
| **11.** | Minada ya hadhara | Tshs 5,000/= |
| **12.** | Miwa | Tshs 3,000/= |
| **13.** | Ushuru wa kupanga meza, kizimba | Tshs 1,000/= |

## SEHEMU D

## USHURU WA MAZAO

| NA. | AINA YA MAZAO | USHURU KWA ASILIMIA |
|---|---|---|
| 1. | Maharage | 3% ya bei ya mauzo |
| 2. | Mchele | 3% ya bei ya mauzo |
| 3. | Alizeti | 3% ya bei ya mauzo |
| 4. | Karanga | 3% ya bei ya mauzo |
| 5. | Mahindi | 3% ya bei ya mauzo |
| 6. | Mpunga | 3% ya bei ya mauzo |
| 7. | Mhogo | 3% ya bei ya mauzo |
| 8. | Vitunguu | 3% ya bei ya mauzo |
| 9. | Nyanya | 3% ya bei ya mauzo |
| 10. | Mtama/uwele | 3% ya bei ya mauzo |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Miwa | 3% ya bei ya mauzo |
| 12. | Dengu | 3% ya bei ya mauzo |
| 13. | Ufuta/ulezi | 3% ya bei ya mauzo |
| 14. | Korosho gunia | 3% ya bei ya mauzo |
| 15. | Matunda | 3% ya bei ya mauzo |
| 16. | Mazao mengine yote ya chakula ambayo hayajaainishwa | 3% ya bei ya mauzo |
| 17. | Mazao mengine yote ya biashara ambayo hayajaainishwa | 3% ya bei ya mauzo |
| 18. | Mazao/mbegu za mazao mengine | 3% ya bei ya mauzo |

**SEHEMU: E**
**USHURU WA NGOZI**

| | **AINA YA NGOZI** | **KIWANGO CHA USHURU** |
|---|---|---|
| **1.** | Ngozi ya ng’ombe | Tshs 500/= kwa kipande |
| **2.** | Ngozi ya mbuzi | Tshs 200/= kwa kipande |
| **3.** | Ngozi ya kondoo | Tshs 200/= kwa kipande |

**SEHEMU: F**
**ADA ZA BURUDANI**

| | AINA YA BURUDANI NAUTAMADUNI | ADA |
|---|---|---|
| 1. | Mziki wa disko | Tshs 20,000/= kwa tukio |
| 2. | Muziki na dansi | Tshs 20,000/= kwa tukio |
| 3. | Burudani ya msanii binafsi | Tshs 30,000/= kwa tukio |
| 4. | Burudani kikundi | Tshs 40,000/= kwa tukio |
| 5. | Taasisi/ kampuni | Tshs 50,000/= kwa tukio |
| 6. | Maigizo ya mazingaombwe kwa siku moja | Tshs 10,000/= kwa tukio |
| 7. | kuonyesha video au sinema kwa siku moja | Tshs 30,000/= kwa tukio |
| 8. | Leseni ndogo kwa waganga wa kienyeji | Tshs 100,000/= kwa mwaka |
| 9. | Matangazo au promosheni | Tshs 30,000/= kwa tukio |
| 10. | Mashindano ya urembo | Tshs 100,000/= kwa tukio |
| 11. | Salon | Tshs 5,000/= kwa mwezi |
| 12. | Wasambazaji wa kebo (cables) | Tshs 10,000/= kwa mwezi |
| 13. | Muziki wa taarabu | Tshs 20,000/= kwa kila tukio |
| 14. | Vituo vya Tv, na radio | Tshs 10,000/= kwa mwezi |
| 15. | Vituo vya magazeti | Tshs 5,000/= kwa mwezi |
| 16. | Mchezo wa puli (pool table) | Tshs 50,000/= kwa mwezi |
| 17. | Wamiliki wa kumbi za burudani | Tshs 10,000/= kwa mwezi |
| 18. | Kupiga picha za video | Tshs 5000/= kwa tukio |
| 19. | Burudani nyinginezo | Tshs 10,000/= kwa kila tukio |
| 20. | Usajili wa vikundi vya Sanaa | Tshs 75,000/=kwa mwaka |
| 21. | Michezo ya bahati nasibu | Tsh 100,000/=kwa mwezi |
| 22. | Mapromota | Tshs 200,000/= kwa mwaka |

**SEHEMU: G**
**ADA YA KIBALI CHA UJENZI KWA MWAKA**

| | AINA YA JENGO | KIASI (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Minara ya simu (telephone tower) | Tshs 250,000/= |
| 2. | Ghorofa (2 stores and above) | Tshs 150,000/= |
| 3. | Nyumba za biashara ( gesti, maduka) | Tshs 50,000/= |
| 4. | Kituo cha mafuta | Tshs 100,000/= |
| 5. | Nyumba za makazi | Tshs 50,000/= |
| 6. | Nyumba za makazi na biasahara | Tshs 50,000/= |
| 7. | Nyumba za biashara | Tshs 50,000/= |
| 8. | Shule binafsi, na Hospitali binafsi | Tshs 100,000/= |
| 9. | Ofisi binafsi | Tshs 100,000/= |
| 10. | Maghala na Bohari | Tshs 100,000/= |
| 11. | Uzio wa ujenzi | Tshs 50,000/= |
| 12. | Kubadili matumizi ya Ardhi | Tshs 50,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| **13.** | Kuhakiki mipaka | Tshs 50,000/= |
| **14.** | Majengo mengine ambayo hayajatajwa | Tshs 20,000/= |

**SEHEMU: H**
**ADA YA MABADILIKO YA JENGO LILILOPO**

| | **AINA YA JENGO** | **KIASI (SHILINGI)** |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya kuishi | Tshs 5,000/= |
| 2. | Nyumba ya biashara | Tshs 10,000/= |
| 3. | Gholofa | Tshs 100,000/= |
| 4. | Kiwanda, bohari, ghala, n.k | Tshs 100,000/= |
| 5. | Majengo mengine ambayo hayajatajwa hapa | Tshs 10,000/= |

## SEHEMU: I
## USHURU WA KULAZA GARI KITUO CHA MABASI

| | **AINA YA GARI** | **ADA** |
|---|---|---|
| 1. | Basi la abiria zaidi 28 | Tshs 5,000/= |
| 2. | Basi la abiria kati ya 20-28 | Tshs 3,000/= |
| 3. | Basi la abiria kati ya 7 – 20 | Tshs 2,000/= |
| 4. | Teksi, Pick up, | Tshs 1,000/= |
| 5. | Magari Binafsi | Tshs 1,000/= |
| 6. | Pikipiki | Tshs 500/= |
| 7. | Baiskeli | Tshs 300/= |
| 8. | Lori zaidi ya tani 10 | Tshs 5,000/= |
| 9. | Lori chini ya tani 10 | Tshs 3,000/= |

**SEHEMU: J**
**ADA YA KUOMBA ZABUNI**

| | **AINA YA ZABUNI** | **ADA** |
|---|---|---|
| **1.** | Uwakala | Tshs 50,000/= |
| **2.** | Zabuni ndogo ndogo | Tshs 100,000/= |
| **3.** | Zabuni za kati | Tshs 150,000/= |
| **4.** | Zabuni kubwa | Tshs 200,000/= |

**SEHEMU: K**
**USHURU WA KITUO CHA MABASI YA ABIRIA**

| | **IDADI YA ABIRIA** | **USHURU KWA SIKU** |
|---|---|---|
| 1. | 4 – 9 | Tshs 1,000/= |
| 2. | 10 – 25 | Tshs 1,000/= |
| 3. | 26 – 35 | Tshs 1,000/= |
| 4. | 66 au zaidi | Tshs 2,000/= |

**SEHEMU: L**
**USHURU WA KUEGESHA MAGARI YA MIZIGO**

| | UZITO WA GARI | USHURU KWA SIKU |
|---|---|---|
| 1. | Chini ya tani3 | Tshs 1,000/= |
| 2. | Tani 3-6 | Tshs 2,000/= |
| 3. | Tani 7-10 | Tshs 3,000/= |
| 4. | Zaidi ya tani 10 | Tshs 5,000/= |

**SEHEMU: M**
**USHURU WA MIFUGO MINADANI**

| | AINA YA MIFUGO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tshs 5,000/= |
| 2. | Mbuzi | Tshs 1,500/= |
| 3. | Kondoo | Tshs 1,500/= |
| 4. | Kuku /Bata | Tshs 200/= |
| 5. | Punda | Tshs 5,000/= |

**SEHEMU: N**

**USHURU WA AINA MBALIMBALI**

| | AINA YA BIDHAA | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| **1.** | Gunia la chumvi | Tshs 500/= |
| **2.** | Gunia la pumba | Tshs1,000/= |
| **3.** | Gunia la mashudu | Tshs 1,000/= |
| **4.** | Kampuni ya upimaji udongo kwa heka | Tshs 5,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya* kanuni ya *11)*

HATI YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi ……………………………..…… nakiri mbele ya ………….ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuri ya Wilaya ya Mkalama, kwamba tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama za Mwaka 2020. Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hizi badala ya kushtakiwa Mahakamani

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KWA KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi………… Mwaka ………………….

*Jina………………………………..* *Saini…………………………………….*

Mbele ya :

Jina: ……………………………………………

Cheo: ………………………………………….

Saini: …………………………………………..